

Africa Inland Church Tanzania

KURUGENZI YA HUDUMA ZA AFYA
CHUO CHA SAYANSI ZA AFYA KOLANDOTO

S.L.P 16, KOLANDOTO
SHINYANGA
TANZANIA



Barua pepe: info@kchs.ac.tz
Simu: +255 625 974142
Tovuti: www.kchs.ac.tz

Kumb Na: KCHS/ADM/20/457

11/11/2020

Mkuu wa Chuo cha Sayansi za Afya Kolandoto kilichopo chini ya Kanisa la Africa Inland Church Tanzania lenye makao makuu yake jijini Mwanza anawatangazia watazania wenye sifa za kujaza nafasi ya kufundisha (WAKUFUNZI) kwa upande wa Madaktari na Wafamasia wenye uwezo wa kufundisha masomo ya Utabibu na Famasia.

Maombi ya kazi yatumwe kwenye barua pepe: info@kchs.ac.tz Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 25 Novemba 2020 saa 10 jioni.

Maombi yaambatanishwe na nyaraka zifuatazo:-

1. Wasifu (CV) wa muombaji.
2. Nakala za vyeti vya Taaluma.
3. Nakala ya matokeo halisi (Transcript)
4. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
5. Nakala ya cheti cha usajili kutoka baraza la Madaktari na Wafamasia.

1.0 DAKTARI DARAJA II (MKUFUNZI) – NAFASI 1

1.1 MAJUKUMU YA MWOMBAJI

- Kufundisha wanafunzi kada ya utabibu hadi hatua ya 6 (NTA 6)
- Kuwaelekeza wanafunzi wadini (kuwafundisha kwa vitendo)
- Kutunga na kusahihisha mitihani yote ya ndani.
- Kusimamia mitihani yote ya ndani na nje wadini.
- Kuwasaidia wanafunzi wanapohitaji msaada wa kitaaluma wakati wote.
- Na majukumu yote utakayopewa na msimamizi wako.

1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

- Mwombaji awe na shahada ya udaktari kutoka chuo kinachotambuliwa na serkali.
- Mwombaji awe mtanzania.
- Mwombaji awe mtifu na mwenye kujituma katika kazi.
- Mwombaji awe na uwezo wa kuandika na kujieleza katika lugha ya Kiwashili na Kiingereza kwa ufasaha.
- Mwombaji awe na uwezo wa kufundisha wanafunzi wa Utabibu kwa nadharia na vitendo.
- Madaktari wanawake wanashauriwa kuomba na watapewa kipaumbele.
- Awe na utayari wa kufanya kazi za ziada pale zinapojitokeza.

1.3 MSHAHARA

Ngazi ya mshahara ni TGHS E1



2.0 MFAMASIA DARAJA II (MKUFUNZI) – NAFASI 1

2.1 MAJUKUMU YA MWOMBAJI

- Kufundisha wanafunzi kada ya famasia hadi hatua ya 6 (NTA 6)
- Kuwaelekeza wanafunzi katika maabara (kuwafundisha kwa vitendo)
- Kutunga na kusahihisha mitihani yote ya ndani.
- Kusimamia mitihani yote ya ndani na nje.
- Kuwasaidia wanafunzi wanapohitaji msaada wa kitaaluma wakati wote.
- Na majukumu yote utakayopewa na msimamizi wako.

2.2 SIFA ZA MWOMBAJI

- Mwombaji awe na shahada ya ufamasia kutoka chuo kinachotambuliwa na serkali.
- Mwombaji awe mtanzania.
- Mwombaji awe mtifu na mwenye kujituma katika kazi.
- Mwombaji awe na uwezo wa kujieleza katika lugha ya Kiwashili na Kiingereza kwa ufasaha.
- Mwombaji awe na uwezo wa kufundisha wanafunzi wa Ufamasia kwa nadharia na vitendo.
- Awe na utayari wa kufanya kazi za ziada pale zinapojitokeza.

2.3 MSHAHARA

Ngazi ya mshahara ni TGHS C1

3.0 MFAMASIA MTEKNOLOJIA (MKUFUNZI MSAIDIZI) – NAFASI 1

3.1 MAJUKUMU YA MWOMBAJI


- Kufundisha wanafunzi kada ya famasia hadi hatua ya 5 (NTA 5)
- Kuwaelekeza wanafunzi katika maabara (kuwafundisha kwa vitendo)
- Kutunga na kusahihisha mitihani yote ya ndani.
- Kusimamia mitihani yote ya ndani na nje.
- Kuwasaidia wanafunzi wanapohitaji msaada wa kitaaluma wakati wote.
- Na majukumu yote utakayopewa na msimamizi wako.

3.2 SIFA ZA MWOMBAJI

- Mwombaji awe na stahada ya ufamasia kutoka chuo kinachotambuliwa na serkali.
- Mwombaji awe mtanzania.
- Mwombaji awe mtifu na mwenye kujituma katika kazi.
- Mwombaji awe na uwezo wa kujieleza katika lugha ya Kiwashili na Kiingereza kwa ufasaha.
- Mwombaji awe na uwezo wa kufundisha wanafunzi wa Ufamasia kwa nadharia na vitendo.
- Awe na utayari wa kufanya kazi za ziada pale zinapojitokeza.

3.3 MSHAHARA

Ngazi ya mshahara ni TGHS B1



**MAOMBI HAYA HAYATAHUSISHA WATUMISHI WALIOAJIRIWA NA SERIKALI,
HOSPITALI TEULE ZA HALMASHAURI NA MASHIRIKA YA HIARI AMBAO WANALIPWA
MSHAHARA NA SERIKALI.**

Maombi yote yaelekezwe kwa:-

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Sayansi za Afya Kolandoto,
S.L.P 16,
Kolandoto – Shinyanga.

